# RASIMU YA SERA YA TAIFA YA UNUNUZI WA UMMA

## YALIYOMO

VIFUPISHO ........ iv
DIBAJI ........ v
SURA YA KWANZA........ 1
1.0 Utangulizi ........ 1
1.1 Mfumo wa Ununuzi wa Umma........ 1
1.2 Hali Ilivyo Sasa........ 3
1.2.1 Ukubwa wa Ununuzi wa Umma........3
1.2.2 Utekelezaji wa Ununuzi wa Umma........4
1.2.3 Utawala Bora ........4
1.2.4 Ununuzi kwa Njia ya Kielektroniki........5
1.2.5 Migongano ya Maslahi ........5
1.2.6 Ununuzi katika Sekta ya Ujenzi na Usimamizi wa Mikataba ........6
1.2.7 Ushirikishwaji wa Makundi Maalum ya Jamii ........7
1.2.8 Matumizi ya Rasilimaliwatu ya Ndani katika Uzalishaji........7
1.2.9 Ununuzi wa Bidhaa na Huduma Zinazozalishwa kwa Kutumia Malighafi za Ndani 8
1.2.10 Maendeleo ya Kada ya Ununuzi na Ugavi Serikalini ........8
SURA YA PILI ........ 10
2.0 UMUHIMU WA SERA ........10
2.1 Madhumuni ya Sera ........10
2.2 Dira, Dhima na Malengo ya Sera ........10
2.2.1 Dira........10
2.2.2 Dhima ........10
2.2.3 Malengo ya Sera ........10
2.2.4 Mipaka ya Sera ........11
SURA YA TATU........ 12
3.0 MASUALA, MALENGO NA MATAMKO YA SERA ........ 12

3.1 MASUALA MAHSUSI ..... 12
3.1.1 Suala: Mfumo wa Ununuzi wa Kielektroniki ..... 12
3.1.2 Suala: Migongano ya Maslahi ..... 12
3.1.3 Suala: Ununuzi katika Sekta ya Ujenzi na Usimamizi wa Mikataba ..... 13
3.1.4 Suala: Matumizi ya Rasilimaliwatu ya Ndani katika Uzalishaji ..... 13
3.1.5 Suala: Matumizi ya Malighafi za Ndani ..... 14
3.1.6 Suala: Maendeleo ya Kada ya Ununuzi na Ugavi Serikalini ..... 14
3.1.7 Suala: Utawala bora ..... 15
3.2 MASUALA MTAMBUKA ..... 15
3.2.1 Suala: Uhifadhi wa Mazingira ..... 15
3.2.2 Suala: Ushirikishwaji wa Makundi Maalum ya Jamii ..... 16
SURA YA NNE ..... 17
4.0 MUUNDO WA KISHERIA ..... 17
SURA YA TANO ..... 18
5.0 MUUNDO WA KITAASISI ..... 18
5.1 Muundo wa Kiutekelezaji ..... 18
5.2 Ufuatiliaji na Tathmini ..... 19
5.2.1 Lengo Kuu la Ufuatiliaji na Tathmini ..... 19
5.2.2 Ufuatiliaji ..... 19
5.2.3 Tathmini ..... 19
5.3 Hitimisho ..... 20

**VIFUPISHO**

| | | |
|---|---|---|
| Ega | - | e- Government Agency |
| GPSA | - | Government Procurement Services Agency |
| NEMC | - | National Environment Management Council |
| OECD | - | Organization for Economic Co-operation and Development |
| PE | - | Procuring Entity |
| PPAA | - | Public Procurement Appeals Authority |
| PPRA | - | Public Procurement Regulatory Authority |
| PSPTB | - | Procurement and Supplies Professionals and Technicians Board |
| TAMISEMI | - | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TEHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| WTO | - | World Trade Organization |
| TZS | - | Tanzania Shilligs |
| PMIS | - | Procurment Management Information System |

## DIBAJI

Eneo la ununuzi wa umma ni moja kati ya maeneo yenye matumizi makubwa ya bajeti ya Serikali. Eneo hilo linalohusisha matumizi katika upatikanaji wa bidhaa, kandarasi za ujenzi na huduma, linakadiriwa kuwa na matumizi yanayozidi asilimia 70 ya bajeti ya Serikali. Matumizi hayo makubwa, yanakabiliwa na changamoto nyingi. Changamoto hizo, zimesababisha kuwapo kwa matumizi ya rasilimali za nchi yasiyo na tija.

Katika kipindi cha mwaka 1965 hadi mwaka 2000 ununuzi wa umma ulikuwa ukitekelezwa kwa kufuata mwongozo uliorithiwa kutoka kwa Serikali ya Wakoloni wa Kiingereza uliojulikana kama "Financial Orders Part III, 5th Edition" ya mwaka 1965. Mwongozo huo uliotumika kwa takribani miaka thelathini na mitano, ulionesha upungufu mkubwa wa kiutekelezaji kutokana na kutoendana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kitekinolojia, n.k yaliyokuwa yametokea ulimwenguni katika kipindi chote hicho. Ili kuendana na mabadiliko hayo, Serikali iliona haja ya kuboresha utekelezaji wa shughuli za ununuzi na ugavi kwa kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 3 ya Mwaka 2001.

Mwaka 2004, Serikali iliifanyia marekebisho Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 3 ya Mwaka 2001 baada ya kubaini upungufu mkubwa katika utekelezaji wa sheria hiyo. Marekebisho hayo, yalipelekea kutungwa kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya Mwaka 2004. Sheria hii, ilizipa mamlaka taasisi nunuzi kufanya maamuzi yote ya ununuzi kupitia bodi zao za zabuni. Ili kuboresha utendaji katika sekta ya ununuzi, Serikali kupitia sheria hiyo, ilianzisha mamlaka za usimamizi wa utekelezaji wa ununuzi na ushughulikiwaji wa malalamiko ya wazabuni.

Mwaka 2011, Serikali iliifuta Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya Mwaka 2004 kwa kutunga sheria mpya ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011. Sababu kuu za kutunga sheria hiyo zilikuwa; kuzipa nguvu zaidi za utekelezaji mamlaka za usimamizi wa ununuzi wa umma, kuweka utaratibu wa ununuzi wa vifaa vilivyotumika, kuweka utaratibu wa ununuzi wa bidhaa na huduma mtambuka, kuweka utaratibu wa ununuzi wa dharura, kuweka utaratibu wa ununuzi kwa njia ya kielektroniki, kupunguza urefu wa michakato ya ununuzi, kuongeza viwango vya adhabu kwa wakiukaji wa sheria ya ununuzi, n.k.

Pamoja na mabadiliko hayo, utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma No.7 ya Mwaka 2011 nao umekutana na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo ni; ukubwa wa gharama za uendeshaji wa michakato ya ununuzi, ukubwa wa bei za bidhaa na huduma zinazonunuliwa na taasisi za umma, urefu wa muda wa michakato ya zabuni, kiwango kidogo cha uadilifu, n.k.

Kufuatia changamoto hizo Serikali iliamua kuifanyia marekebisho kwa kuipitisha Sheria ya Ununuzi wa Umma Na.5 ya Mwaka 2016 kama ilivyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Juni 2016.

Pamoja na jitihada hizo za Serikali, utekelezaji wa shughuli za ununuzi umeonesha upungufu unaotokana na kukosekana kwa miongozo mahsusi ya kisera. Upungufu huo, umekuwa ni chanzo cha mabadiliko ya mara kwa mara ya Sheria ya Ununuzi wa Umma na umejitokeza katika maeneo mbalimbali kama; matumizi ya TEHAMA katika ununuzi, usimamizi wa mikataba, migongano ya kimaslahi, ushirikishwaji wa makundi maalum ya kijamii, ukuzaji wa viwanda vya ndani na matumizi ya rasilimaliwatu na malighafi za ndani, n.k. Hali hii, inaonesha umuhimu wa kuandaliwa kwa miongozo ya kisera kupitia Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma. Sera hii itaiimarisha sekta ya ununuzi na kuongeza mchango katika kuleta maendeleo ya Taifa.

Mwisho, ninapenda kuwashukuru wadau walioshiriki kufanikisha ukamilishwaji wa Sera hii.

Dkt. Philip I. Mpango (Mb)
**Waziri wa Fedha na Mipango**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Ununuzi wa Umma ni suala mtambuka linalopaswa kushughulikiwa kwa uangalifu mkubwa kutokana na athari zake katika uchumi wa nchi. Ununuzi wa umma unaweza kuwezesha ama kuzorotesha ufikiwaji wa mipango ya maendeleo ya kitaifa. Kutokana na uwezekano wa kujitokeza kwa athari hizo katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kitaifa, mfumo mzima wa ununuzi wa umma ni muhimu ukaangaliwa kwa kuzingatia athari zake.

## 1.1 Mfumo wa Ununuzi wa Umma

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua umuhimu wa ununuzi katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Serikali inaamini kwamba sera nzuri ya ununuzi inayotekelezeka ina mchango mkubwa katika kupunguza umasikini na kukuza Uchumi wa nchi. Kwa mantiki hiyo, kuanzia katikati ya miaka ya 1990, Serikali imefanya mabadiliko mbalimbali ya mifumo ya ununuzi. Moja ya mambo yaliyotoa msukumo wa mabadiliko hayo ni haja ya kuondoa kasoro kubwa kwenye mfumo wa ununuzi uliokuwepo ambao ulitawaliwa na sheria ambazo hazikuwa toshelevu na zilizokuwa zimetawanyika sana. Kwa mfano, kazi za ununuzi zilikuwa zikitekelezwa kwa mfumo wa ununuzi uliokuwa umetawanyika sana. Mfumo huo ulizihusisha mamlaka mbalimbali bila ya kuwa na uratibu thabiti. Mamlaka hizo ni pamoja na; Bohari Kuu ya Serikali, Bohari ya madawa, Maduka ya Dawa za Mifugo, Bohari ya Maji, Mpiga Chapa wa Serikali na Kitengo cha Ufundi Umeme na Mitambo cha Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano. Serikali ilitunga Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 3 ya mwaka 2001 ambapo ununuzi ulikuwa ukifanyika kupitia Bodi Kuu ya Zabuni hivyo taasisi nunuzi kukosa Mamlaka kamili ya kufanya ununuzi. Kutokana na upungufu huo Serikali iliifuta sheria hiyo na kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya Mwaka 2004. Sheria hii, ilizipa mamlaka taasisi nunuzi kufanya maamuzi yote ya ununuzi kupitia bodi zao za zabuni. Ili kuboresha utendaji katika sekta ya ununuzi, Serikali kupitia sheria hiyo, ilianzisha mamlaka za usimamizi wa utekelezaji wa ununuzi na ushughulikiwaji wa malalamiko ya wazabuni.

Pamoja na jitihada za Serikali za kuondoa mtawanyiko wa taratibu za ununuzi na uboreshaji uliofanyika katika taasisi zinazohusika na ununuzi, bado mchango wa sekta ya ununuzi katika kuchochea maendeleo ya taifa umeendelea kuwa katika kiwango kisichoridhisha, hivyo kushindwa kufikia kiwango cha tija iliyokusudiwa katika ununuzi wa umma unaoendelea kufanywa na Serikali. Kuendelea kufanyika

kwa ununuzi wa umma katika mazingira ambapo kuna kiwango kisichoridhisha cha tija wakati ununuzi wa umma unaofanyika unakadiriwa kuwa na wastani wa kati ya asilimia 60 hadi 70 ya matumizi yote ya Serikali, ni wazi kwamba malengo ya Serikali ya kuitumia sekta ya ununuzi wa umma kuwa kichocheo cha maendeleo ya taifa hayataweza kufikiwa, na hivyo kuinyima Serikali fursa muhimu ya kuutumia vizuri mfumo wa ununuzi wa umma kwa manufaa ya Taifa.

Zipo sababu mbalimbali zinazochangia kuendelea kuwepo kwa hali hii ambazo ni pamoja na; sheria zilizopo kushindwa kuakisi mahitaji halisi ya sekta ya ununuzi; Kuwepo kwa mabadiliko mbalimbali yanayoendelea kujitokeza katika sekta ya umma hapa nchini na duniani kwa ujumla. Mfano, mabadiliko ya kiteknolojia ambapo ununuzi wa umma haujatumia fursa ya ukuaji wa teknolojia katika kuwezesha kuwepo kwa tija katika sekta hii. Mabadiliko ya kisiasa, kijamii, na Utawala Bora ni baadhi ya sehemu ya masuala yanayoguswa katika sekta ya ununuzi. Maeneo hayo yanapaswa kupewa kipaumbele katika mazingira ya ushindani wa kisiasa unaochangiwa na kuwepo kwa uelewa mkubwa katika jamii wa kudai uwajibikaji Serikalini. Vilevile mabadiliko ya kiuchumi na matumizi bora ya rasilimali za ndani ya nchi hayajaakisiwa katika sekta ya ununuzi wa umma pamoja na ukweli kwamba sekta hii ni mtambuka ambayo inaweza kuleta mguso mpana katika matumizi bora ya rasilimali za ndani. Kupitia mfumo wa ununuzi rasilimali hizi zinaweza kutumika kama egemeo la Serikali kwenye ukuzaji wa uchumi wa nchi.

Pamoja na kuwepo kwa sababu hizi, Serikali haijawahi kuwa na sera rasmi ya ununuzi umma ili kutoa mwongozo maalum wa kisera unaofafanua malengo na nia ya Serikali katika utekelezaji wa jukumu hili muhimu kwa Taifa. Ununuzi wa umma umeendelea kutawaliwa na sheria ambazo zimeonyesha upungufu wakati wa utekelezaji wake. Upungufu uliopo katika sheria zinazotawala mfumo wa ununuzi pamoja na mabadiliko mbalimbali yanayoendelea kutokea umeleta pengo katika mfumo wa ununuzi. Kutokana na hali hii ni dhahiri ipo haja ya kuwa na mtizamo mpana ambao utaweka msingi wa namna bora ya kushughulikia upungufu uliopo na mabadiliko yanayoendelea kutokea. Katika muktadha huu, kuna umuhimu wa kuwa na Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma. Aidha, haja ya kuwa na Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma inachangiwa pia na azma ya Serikali ya kuyawezesha makundi mbalimbali katika jamii kama Vijana, Wazee, wanawake na walemavu kushiriki katika uchangiaji wa uchumi. Pia kuendelea kufanyika kwa marekebisho ya Sheria ya ununuzi ya mara kwa mara yanaashiria kuwa kuna umuhimu wa kuwa na maelekezo ya kisera yatakayotoa mwongozo wa utekelezaji wa Sheria. Kutokana na kuendelea kuwepo kwa pengo hilo, sera hii inatungwa kwa lengo la kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo. Vilevile, sera hii inatungwa

ikizingatia jitihada za dhahiri za Serikali zenye nia ya kuleta mabadiliko katika sekta ya ununuzi wa umma ili kufanya ununuzi uwe wa manufaa kwa taifa la Tanzania kwa kusaidia kuleta usawa wa kijamii miongoni mwa makundi mbalimbali, kukuza viwanda vya ndani, na kutoa fursa kwa wananchi kumiliki uchumi na kuchangia pato la taifa.

## 1.2 Hali Ilivyo Sasa

### 1.2.1 Ukubwa wa Ununuzi wa Umma

Ukubwa wa ununuzi wa umma unaweza kuonekana kwa kuangalia kiasi cha fedha kinachotumika ikilinganishwa na pato la Taifa, ukubwa wa matumizi serikalini na bajeti ya serikali. Kwa mfano, takwimu za utafiti wa ulinganisho wa ununuzi wa umma kwa nchi kumi uliofanywa na Benki ya Dunia (2015), zinaonesha kuwa nchi zinazoendelea hutumia wastani wa Dola za Kimarekani bilioni 820 kwa mwaka katika ununuzi wa umma. Huu ni wastani wa asilimia 15 hadi 20 ya pato la taifa kwa nchi zinazoendelea. Katika nchi changa kiuchumi kama Tanzania, ununuzi wa umma unakadiriwa kuwa na wastani wa kati ya asilimia 60 hadi 70 ya matumizi yote ya Serikali. Katika nchi za Jumuiya ya Ushirikiano wa Kimaendeleo (OECD), ununuzi wa umma hutumia takribani ya theluthi moja ya matumizi yote ya Serikali.

Nchini Tanzania, matumizi ya fedha kupitia ununuzi wa bidhaa na huduma yanachukua nafasi ya kwanza baada ya kutoa mishahara. Kwa mujibu wa Taarifa za Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kati ya mwaka wa fedha wa 2007/08 hadi 2014/15, zinaonesha kwamba baadhi ya taasisi zilizokaguliwa katika kipindi hicho ziliingia mikataba ya ununuzi yenye thamani ya TZS trilioni 1.800 (2007/08), TZS trilioni 2.963 (2008/09), TZS trilioni 3.075 (2009/10), TZS trilioni 4.532 (2010/11), TZS trilioni 4.325 (2011/12), TZS trilioni 4.884 (2012/13), TZS trilioni 4.859 (2013/14) na TZS trilioni 4.349 (2014/15). Taarifa hizo zinathibitisha kuwa sehemu kubwa ya bajeti ya Serikali hutumika kwenye ununuzi.

Aidha, utafiti uliofanywa hapa nchini na Crown Agents (1992), ulibainisha athari zinazotokana na kukosekana kwa sera ya taifa ya ununuzi nchini. Halikadhalika, utafiti uliofanyika nchini Kenya (Ngwili na Were, 2014) kuhusu masuala yanayoathiri ufanisi katika ununuzi, ulibaini kuwa ununuzi wa umma una mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi katika nchi yeyote, hivyo kutakiwa kuwekewa miongozo mahsusi ili kuisaidia serikali kufikia malengo ya kiuchumi na kimaendeleo. Vilevile, utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia (2015) kuhusu ulinganisho wa ununuzi wa umma kwa nchi kumi duniani, ulionesha kuwa kiwango cha matumizi kupitia ununuzi wa umma kimeendelea kuongezeka. Kwa

mfano, kati ya mwaka 2006 hadi 2010 ununuzi katika Jumuiya ya Ulaya uliongezeka kwa asilimia 62.

### 1.2.2 Utekelezaji wa Ununuzi wa Umma

Mfumo uliopo wa ununuzi wa umma unaongozwa na Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 iliyoanza kutumika rasmi kupitia Tangazo la Serikali Na. 446 la tarehe 20 Desemba, 2013. Hivyo, kuanzia tarehe hiyo, taasisi zote za umma zilitakiwa kufanya ununuzi kwa kutumia Sheria hiyo na Kanuni zake.

Utekelezwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma unazingatia miongozo inayotolewa na Serikali kupitia Wizara yenye dhamana ya usimamizi wa ununuzi wa umma. Miongozo ya jinsi ya kuandaa mipango ya ununuzi, zabuni, mapokezi ya vifaa/huduma, ununuzi wa jumla wa vifaa, ushughulikiwaji wa malalamiko ya washiriki wa zabuni za umma, n.k imekuwa ikitolewa kwa taasisi nunuzi kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Kwa upande mwingine, Serikali kupitia vyombo vyake vya ukaguzi, hufanya ukaguzi wa utekelezaji wa ununuzi wa umma katika taasisi zake. Ukaguzi huu kwa kiasi kikubwa hulenga uzingatiwaji wa Sheria, Kanuni na taratibu za ununuzi wa umma. Matokeo ya kaguzi hizo, hutumika katika kuboresha utekelezaji na uwajibikaji.

### 1.2.3 Utawala Bora

Suala la utawala bora linahitaji kupewa kipaumbele katika ununuzi wa umma. Utawala bora unaangaliwa katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwajibikaji, uwazi na uzingatiwaji wa Sheria kwa lengo la kupata thamani halisi ya fedha katika ununuzi wa umma. Katika kuhakikisha suala la utawala bora linazingatiwa katika ununuzi wa umma, Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali zikiwa ni pamoja na kuandaa mapendekezo ya Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya ununuzi. Katika kikao cha tatu cha Bunge la kumi na moja la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kilipitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa kurekebisha vifungu vilivyokuwa vikwazo katika utekelezaji wa ununuzi.

Ili kuhakikisha uwajibikaji katika ununuzi wa umma, Serikali imeweka mfumo wa usimamizi na udhibiti kwa kuanzisha vyombo mbalimbali. Vyombo hivyo vinatekeleza majukumu yafuatayo: masuala ya kisera na usimamizi wa maendeleo ya kada ya ununuzi na ugavi serikalini; udhibiti wa ununuzi wa umma; ushughulikiwaji wa malalamiko ya wazabuni; usimamizi wa mikataba ya ununuzi na usambazaji wa bidhaa na huduma mtambuka; usajili na uendelezaji wa

taaluma ya ununuzi na ugavi nchini; na utekelezaji wa shughuli za ununuzi na ugavi katika taasisi za umma.

Pamoja na jitihada hizo za Serikali, suala la utawala bora katika ununuzi wa umma umekuwa si wa kuridhisha. Kwa mfano, kaguzi zilizofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma mwaka 2006 hadi 2011, zinaonesha wastani wa ongezeko la uzingatiaji wa sheria kuwa ni asilimia 7.25; na kwa kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015, ongezeko la uzingatiaji wa sheria ni wastani wa asilimia 0.25.

**Changamoto**

Kasi ndogo ya uzingatiwaji wa sheria katika nunuzi za umma zinazofanyika na kusababisha kuendelea kutotekelezwa kwa zabuni za umma ipasavyo

### 1.2.4 Ununuzi kwa Njia ya Kielektroniki

Ukuaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ni fursa muhimu katika kuleta tija katika sekta ya ununuzi wa umma. Mfano Ununuzi kwa njia ya kielektroniki ni moja ya njia za kisasa katika ununuzi yenye lengo la kuongeza ufanisi kwa kuongeza kasi ya utekelezaji na uwazi, kupunguza gharama na mianya ya rushwa, n.k. Ili kunufaika na matumizi ya njia hii ya ununuzi, Serikali imeandaa mazingira wezeshi kwani imeanzisha mifumo mbalimbali yenye lengo la kuhakikisha ununuzi unafanyika kwa uwazi na ufanisi ikiwemo: tovuti (website); tovuti maalum ya zabuni (tenders portal); mfumo wa taarifa za ununuzi (Procurement Management Information System - PMIS) ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za ununuzi. Taarifa hizo ni pamoja na; matangazo ya zabuni, mikataba ya ununuzi, mipango ya ununuzi ya mwaka ya taasisi za umma, taarifa mbalimbali za utekelezaji wa sheria ya ununuzi, n.k. Pamoja na kuwapo kwa jitihada hizo, mfumo uliopo umejikita zaidi katika utoaji wa taarifa na kuyaacha maeneo mengine ya utekelezaji wa ununuzi wa umma, hivyo kuathiri juhudi za Serikali za kuongeza ufanisi katika ununuzi.

**Changamoto**

Kukosekana kwa mwongozo mahsusi wa matumizi ya TEHAMA katika sekta ya ununuzi wa umma.

### 1.2.5 **Migongano** ya **Maslahi**

Migongano ya maslahi ni hali inayotokana na tofauti za kimatarajio miongoni mwa wadau wa jambo moja. Tofauti hizo, husababisha wadau husika kufanya jitihada za kuyafikia malengo yao bila ya kuzingatia athari za kimaslahi zinazoweza kuwapata wadau wengine. Migongano hiyo, hujitokeza zaidi katika

shughuli zinazohusika na matumizi ya rasilimali za nchi ikiwemo ununuzi wa umma. Migongano ya kimaslahi ina athari kubwa katika kuyafikia malengo ya Serikali katika ununuzi.

Ili kupata matokeo yaliyokusudiwa katika ununuzi wa umma, Serikali imeweka miongozo ya kisheria na kikanuni yenye lengo la kupunguza migongano ya kimaslahi katika ununuzi wa umma. Hata hivyo, suala hili limeendelea kuwa ni changamoto katika utekelezaji wa ununuzi nchini.

**Changamoto**

Kukosekana kwa mwongozo utakaoelekeza namna ya kupunguza migongano ya kimaslahi katika ununuzi wa umma. (Nafikiri tutafute kama kuna changamoto nyingine ipo au tutajadili kwa namna gani)

### 1.2.6 Ununuzi katika Sekta ya Ujenzi na Usimamizi wa Mikataba

Sekta ya ujenzi ni sekta muhimu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Ununuzi katika sekta hii unahitaji usimamizi madhubuti kwa kuwa kiasi kikubwa cha fedha za maendeleo zinazotengwa katika bajeti ya Serikali hutumika katika kuendeleza miundombinu ya nchi. Kwa mfano, taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonesha kuwa, katika mwaka wa fedha (2007/08), kiasi cha TZS trilioni 1.800 na TZS trilioni 4.349 kwa mwaka wa fedha (2014/15) zilitumika katika mikataba ya ununuzi. Ununuzi katika sekta ya ujenzi na usimamizi wa mikataba unatekelezwa kwa kutumia Sheria ya Ununuzi wa Umma SURA 410, ambapo taasisi nunuzi zinapaswa kuzingatia sheria hiyo katika utekelezaji wa ununuzi wa kandarasi za ujenzi na usimamizi wa mikataba. Aidha, Serikali imeendelea na jitihada za kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa ununuzi katika sekta ya ujenzi zenye lengo la kuhakikisha upatikanaji wa thamani halisi ya fedha zilizotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo. Hata hivyo, utekelezaji wa shughuli hiyo umebainisha upungufu kama taarifa za ukaguzi wa ununuzi zinavyoonesha (CAG 2012/13; PPRA, 2014/15). Upungufu huo ni pamoja na: ukadiriaji muda na gharama usio halisi, ongezeko la gharama wakati wa utekelezaji wa miradi, ukosefu wa uhakika wa ubora katika hatua ya mipango, ukosefu wa mipango ya ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa miradi, usanifu usiotosheleza wa miradi ya ujenzi n.k. Vilevile, tathmini iliyofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango mwaka 2014/15, kupitia mtaalam mwelekezi kuhusu mahitaji ya mafunzo kwa maafisa ununuzi na ugavi serikalini, ilibaini kuwapo kwa kiwango kidogo cha uelewa wa masuala ya usimamizi wa mikataba. Ambapo asilimia 6.4 ya maafisa ununuzi na ugavi 94 waliopo katika Serikali Kuu wameonesha kuwa na uelewa na uzoefu wa kutosha katika eneo hilo hivyo kuhitaji kuwekewa mkazo zaidi.

### Changamoto

Kukosekana kwa mwongozo mahsusi wa ununuzi katika sekta ya ujenzi na usimamizi wa mikataba.

### 1.2.7 Ushirikishwaji wa Makundi Maalum ya Jamii

Ushiriki wa makundi maalum ya kijamii katika ununuzi wa umma ni muhimu katika ustawi wa jamii na kukuza uchumi wa nchi. Hapa nchini, kumekuwepo na ushiriki mdogo wa makundi yanayojumuisha vijana, wazee, wanawake, wajasiriamali wadogo na watu wenye mahitaji maalum katika zabuni za umma. Hii inatokana na sababu mbalimbali ikiwamo, upatikanaji wa taarifa za zabuni, uwezo wa makundi hayo kushiriki, n.k. Hali hii, inayanyima fursa za uchangiaji wa makundi hayo katika ukuaji wa uchumi wa makundi yenyewe na Taifa kwa ujumla.

Kwa kutambua umuhimu wa makundi hayo, Serikali imeendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha kuwa mazingira yanaandaliwa ili kuyawezesha makundi hayo kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Kupitia sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi makundi haya yameendelea kushirikishwa katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya kisekta. Pia Sheria ya Ununuzi wa Umma inaelekeza ushiriki wa makundi hayo katika zabuni za umma. Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa sheria inayosisitiza ushiriki wa makundi hayo katika ununuzi wa umma, bado kiwango cha ushiriki wa makundi hayo si cha kuridhisha.

**Changamoto:**

kukosekana kwa mwongozo mahsusi unaolenga kuongeza ushirikishwaji wa makundi maalum ya kijamii katika zabuni za umma.

### 1.2.8 Matumizi ya Rasilimaliwatu ya Ndani katika Uzalishaji

Matumizi ya rasilimaliwatu ya ndani katika makampuni yanayoshiriki katika zabuni za umma ni muhimu katika kujenga uwezo wa wananchi na pia kukuza uchumi. Hapa nchini, ushiriki wa makampuni yanayotumia rasilimaliwatu ya ndani katika uzalishaji kwenye zabuni za umma ni mdogo. Kutokana na hali hiyo, Serikali, kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016, imeweka upendeleo maalum kwa makampuni yanayomilikiwa na wananchi na pia yanayomilikiwa kwa ushirikiano kati ya wazawa na wageni katika kazi za ujenzi au za ushauri . Hata hivyo, mwongozo huo wa kisheria, unahusu umiliki wa makampuni pekee bila ya kuhusisha matumizi ya rasilimaliwatu ya ndani.

**Changamoto**

Kukosekana kwa mwongozo mahsusi unaoelenga kuongeza matumizi ya rasilimaliwatu ya ndani katika shughuli za kiuchumi hususan za ununuzi wa umma.

### 1.2.9 Ununuzi wa Bidhaa na Huduma Zinazozalishwa kwa Kutumia Malighafi za Ndani

Ununuzi wa bidhaa na huduma zinazozalishwa kwa kutumia malighafi za ndani, ni njia muhimu ya kujenga uwezo wa kiuchumi wa wananchi wanaoshiriki katika kuzalisha malighafi hizo. Pamoja na kujenga uwezo wa kiuchumi, matokeo ya ununuzi huo yana mchango mkubwa kwa maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Hapa nchini, ununuzi wa bidhaa na huduma zinazozalishwa kwa kutumia malighafi za ndani kwa matumizi ya Serikali, bado ni wa kiwango cha chini. Kutokana na hali hiyo, Serikali kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya mwaka 2011 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016, imeweka msisitizo wa ununuzi wa bidhaa na huduma zinazozalishwa kwa kutumia malighafi za ndani wenye lengo la kuhamasisha ukuaji wa viwanda vya ndani. Hata hivyo, ununuzi wa bidhaa mbalimbali kwa matumizi ya taasisi za umma kama samani, sare, vyakula, mapambo, vifaa vya ujenzi, n.k bado hauzingatii azma hiyo ya Serikali.

**Changamoto**

Kukosekana kwa mwongozo mahsusi unaolenga kukuza ushiriki wa wazalishaji wa bidhaa na huduma zinazotumia malighafi za ndani.

### 1.2.10 Maendeleo ya Kada ya Ununuzi na Ugavi Serikalini

Maendeleo ya kada ya ununuzi na ugavi serikalini ni muhimu katika utekelezaji wa shughuli za ununuzi wenye tija. Kama ilivyo kwa kada zingine, kukosekana kwa kada imara ya ununuzi, ni jambo lenye madhara makubwa katika utekelezaji na pia kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa. Kwa kuzingatia ukweli kwamba sehemu kubwa ya matumizi ya bajeti ya Serikali hufanyika kupitia ununuzi, suala la weledi, likijumuishwa na uwepo wa mazingira wezeshi ya utendaji kazi, ni muhimu katika kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa kwa ufanisi.

Hapa nchini, ufanisi wa ununuzi wa umma unaathiriwa na mambo mbalimbali ikiwamo kukosekana kwa kada imara ya ununuzi na ugavi serikalini. Katika kukabiliana na hali hiyo, jitihada mbalimbali zimeendelea kufanyika. Moja ya jitihada hizo ni kuanzishwa kwa Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi nchini. Ambapo, kuanzia mwaka 2011 hadi kufikia Aprili 2016, jumla ya wataalam 5175 walikuwa wamehitimu na kusajiliwa katika ngazi mbalimbali za kitaaluma. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2011 hadi Juni, 2016, jumla ya taarifa za watumishi

3400 wanaofanya kazi za ununuzi na ugavi katika ofisi za umma zimeorodheshwa katika daftari la maafisa ununuzi na ugavi lililopo Wizara ya Fedha na Mipango. Kati ya hao, maafisa 838 (24.6%) ndiyo wenye sifa ya taaluma ya ununuzi na ugavi. Wizara pia ilifanya tathmini kuhusu mahitaji ya mafunzo kwa maafisa ununuzi na ugavi waliopo serikalini (2013-2015), na kubainisha kuwepo kwa mahitaji makubwa ya kujengewa uwezo katika maeneo yanayohusiana na; usimamizi wa mikataba, majadiliano katika mikataba (negotiation); ununuzi wa kielektroniki na usimamizi wa vihatarishi. Aidha, utafiti huo pia ulibainisha kuwepo kwa upungufu wa idadi ya maafisa ununuzi na ugavi, ikilinganishwa na mahitaji ya ofisi hizo. Kwa upande mwingine, taarifa ya utekelezaji ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013/14, imebainisha kuwapo kwa upungufu wa kitaaluma miongoni mwa watendaji wa ununuzi na ugavi.
Katika jitihada za kukabiliana na upungufu huo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali. Hatua hizo ni pamoja na kutoa mafunzo ya uelewa wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, kudhamini watumishi wake katika taasisi mbalimbali za mafunzo, kuandaa warsha na makongamano, n.k. Pamoja na jitihada hizo, bado upungufu umeendelea kuwepo na hivyo kuathiri utendaji na maendeleo ya kada hiyo kwa ujumla.

**Changamoto**

Kukosekana kwa miongozo mahsusi inayoratibu jitihada za Serikali za kuendeleza kada ya ununuzi na ugavi.

# SURA YA PILI

## 2.0 UMUHIMU WA SERA

### 2.1 Madhumuni ya Sera

Madhumuni ya Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma ni kuandaa mazingira wezeshi ili yawe kichocheo cha maendeleo ya Taifa na ustawi wa watu wake. Uhalali wa sera hii upo katika azma yake ya kukuza ustawi wa Taifa letu. Kwa kuzingatia kuwa zaidi ya asilimia 70 ya Bajeti ya Serikali hutumika katika ununuzi wa bidhaa, kandarasi za ujenzi na huduma, kuna umuhimu wa kuwa na maelekezo ya kisera yatakayotoa mwongozo na kuweka misingi ya utekelezwaji wa sheria, kanuni na taratibu zitakazozingatiwa ili kutoa mchango unaokusudiwa kwa Taifa. Sera inakusudia kutoa maelekezo kuhusu:uadilifu miongoni mwa washiriki wa ununuzi wa umma; ufanisi katika ununuzi unaofanywa na taasisi za umma; ushirikishwaji wa wajasiriamali wadogo na wa kati pamoja na makundi maalumu ya kijamii katika zabuni za umma; mikakati ya kukuza makampuni ya ndani kupitia ununuzi wa umma; usimamizi thabiti wa mikataba na ununuzi katika sekta ya ujenzi; mfumo wa ununuzi wa kielektroniki; matumizi ya kutosha ya rasilimaliwatu ya ndani katika uzalishaji; ununuzi wa bidhaa zinazozalishwa kwa malighafi za ndani; utawala bora katika ununuzi wa umma; mfumo endelevu wa uhifadhi wa mazingira katika ununuzi; na kudhibiti mgongano wa kimaslahi miongoni mwa wadau wa ununuzi wa umma.

### 2.2 Dira, Dhima na Malengo ya Sera

#### 2.2.1 Dira

Kujenga ushindani, usawa, uwazi, uwajibikaji na ubora wa kazi katika mfumo wa ununuzi wa umma nchini.

#### 2.2.2 Dhima

Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma itahimiza uzingatiaji wa misingi ya ununuzi ambayo ni uwazi, uwajibikaji, uadalifu, ushindani wa haki na upatikanaji wa thamani halisi ya fedha iliyotumika ili kujenga mfumo wa ununuzi wa umma wenye manufaa kwa Taifa.

#### 2.2.3 Malengo ya Sera

**Lengo Kuu la Sera**

Lengo kuu la sera hii ni kutekeleza ununuzi wa umma kwa ufanisi chini ya usimamizi madhubuti wenye kuzingatia uadilifu, usawa, uwazi, uwajibikaji, uhifadhi wa mazingira na utawala bora.

**Malengo Mahsusi ya Sera**

Malengo mahsusi yatakayotumika katika utekelezaji wa sera ni kama ifuatavyo:-

a) Kuhakikisha ununuzi wa umma unazingatia misingi ya utawala bora;

b) Kuhakikisha ununuzi hauna madhara au matokeo hasi katika utunzaji wa mazingira;

c) Kutoa fursa za upendeleo kwa makundi maalum ya kijamii na kujenga uwezo kwa makampuni ya ndani na wajasiriamali wadogo kushiriki katika zabuni za umma;

d) Kuhimiza matumizi ya TEHAMA katika ununuzi wa umma;

e) Kuendeleza kada ya ununuzi na ugavi nchini.

f) Kudhibiti migongano ya kimaslahi miongoni mwa wadau wa ununuzi wa umma;

g) Usimamizi madhubuti wa mikataba ya ununuzi pamoja na sekta ya ujenzi;

h) Kuhamasisha matumizi ya rasilimaliwatu ya ndani katika uzalishaji; na

i) Kuhimiza matumizi ya bidhaa na huduma zinazozalishwa kwa kutumia malighafi za ndani.

### 2.2.4 Mipaka ya Sera

Sera hii inahusu ununuzi katika taasisi zote za umma. Pia inahusu ununuzi unaofanywa na taasisi binafsi kwa kutumia fedha za umma. Halikadhalika, ununuzi wa aina yoyote (wa umma au sekta binafsi) utakaohusu kuokoa uhai wa viumbe, mazingira na utunzaji wa mfumo wa ikolojia utatakiwa kuzingatia sera hii. Sheria, kanuni na taratibu zitakazotokana na sera hii, zitalazimika kuonesha kama aina ya ununuzi ni mahsusi kwa bidhaa, kandarasi za ujenzi na huduma pamoja na mambo ya kimkakati na yanayohusu usalama.

# SURA YA TATU

## 3.0 MASUALA, MALENGO NA MATAMKO YA SERA

## 3.1 MASUALA MAHSUSI

### 3.1.1 Suala: Mfumo wa Ununuzi wa Kielektroniki

**Maelezo**

Tekinolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ni nyenzo muhimu katika kuleta ufanisi wa shughuli mbalimbali. Mifumo ya TEHAMA imeonesha mafanikio makubwa katika sekta zote ikiwemo sekta ya ununuzi wa umma. Matokeo ya tekinolojia hiyo, yamejidhihirisha katika maeneo mengi yakiwamo; kuongeza uwazi na wigo wa upatikanaji wa taarifa, kupunguza muda na gharama za utekelezaji, n.k. Hata hivyo, matumizi ya TEHAMA katika ununuzi wa umma hapa nchini ni ya kiwango kidogo ambapo kwa kiasi kikubwa yametokana na kukosekana kwa miongozo mahsusi ya kisera na hivyo kuikosesha Serikali kunufaika na faida zitokanazo na mfumo huo.

**Lengo**

Kuwa na mfumo wa kielektroniki wenye kuleta ufanisi katika ununuzi wa umma.

**Tamko la sera**

Serikali itaweka mwongozo utakaobainisha malengo mahsusi yanayokusudiwa katika kuleta ufanisi kwa kutumia ununuzi kwa njia ya kielektroniki;

### 3.1.2 Suala: Migongano ya Maslahi

**Maelezo**

Migongano ya maslahi miongoni mwa wahusika wa ununuzi wa umma ni jambo lisiloepukika. Migongano hiyo husababishwa na matarajio tofauti ya wahusika wa jambo moja. Katika shughuli zote zinazohusisha matumizi ya rasilimali kama fedha, madini, maliasili, n.k huvuta wadau wengi wenye mitazamo na matarajio tofauti na hivyo kusababisha kuwapo kwa migongano ya maslahi. Ununuzi wa umma ni moja ya shughuli zenye kuhusisha wadau wengi na hivyo kuwapo kwa migongano mingi ya maslahi yenye athari kubwa katika kufikia malengo yaliyokusudiwa. Hata hivyo, katika ununuzi wa umma hapa nchini, kumekuwepo na migongano ya aina hiyo. Mfano mmojawapo wa migongano hiyo ni ile inayohusu maslahi binafsi dhidi ya maslahi ya taasisi au Serikali kwa ujumla. Migongano hii isipodhibitiwa huwa na madhara makubwa.

**Lengo**
Kudhibiti migongano ya maslahi katika ununuzi wa umma.

**Tamko la sera**
Serikali itaandaa mwongozo dhidi ya maslahi binafsi katika ununuzi wa umma ili kupunguza madhara ya migongano ya kimaslahi.

### 3.1.3 Suala: Ununuzi katika Sekta ya Ujenzi na Usimamizi wa Mikataba

**Maelezo**
Sekta ya ujenzi na usimamizi wa mikataba ni muhimu katika kuendeleza miundombinu ambayo inawezesha utekelezwaji wa shughuli za kimaendeleo. Sekta hii hutumia kiasi kikubwa cha fedha ikilinganishwa na sekta zingine za umma na hivyo kuhitaji usimamizi madhubuti. Hata hivyo, kumekuwepo na changamoto za kiutekelezaji katika sekta hiyo ambazo huisababishia Serikali hasara za mara kwa mara.

**Lengo**
Kuwa na mwongozo mahsusi wa ununuzi katika sekta ya ujenzi na usimamizi wa mikataba.

**Tamko la sera**
Serikali itachukua hatua mahsusi za kusimamia utekelezaji wa Ununuzi katika sekta ya ujenzi na kuimarisha usimamizi wa mikataba ili kupata thamani halisi ya fedha.

### 3.1.4 Suala: Matumizi ya Rasilimaliwatu ya Ndani katika Uzalishaji

**Maelezo**
Matumizi ya rasilimaliwatu ya ndani katika makampuni yanayoshiriki katika zabuni za umma ni muhimu katika kujenga uwezo wa wananchi na pia kukuza uchumi. Hapa nchini, ushiriki wa makampuni yanayotumia rasilimaliwatu ya ndani katika uzalishaji kwenye zabuni za umma ni mdogo, hivyo, kuongeza matabaka na ukosefu wa ajira miongoni mwa jamii.

**Lengo**
Kuongeza kiwango cha matumizi ya rasilimaliwatu ya ndani katika viwanda na makampuni yanayoshiriki katika zabuni za umma.

**Tamko la sera**
Serikali itachukua hatua mahsusi za kuhakikisha kunakuwepo na matumizi stahiki ya rasilimaliwatu ya ndani katika uzalishaji ili kuongeza ajira kwa watanzania.

### 3.1.5 Suala: Matumizi ya Malighafi za Ndani

**Maelezo**
Ununuzi wa bidhaa na huduma zinazozalishwa kwa kutumia malighafi za ndani, ni njia muhimu ya kujenga uwezo wa kiuchumi wa wananchi wanaoshiriki katika kuzalisha malighafi hizo. Pamoja na kujenga uwezo wa kiuchumi, matokeo ya ununuzi huo yana mchango mkubwa kwa maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Hapa nchini, ununuzi wa bidhaa na huduma zinazozalishwa kwa kutumia malighafi za ndani kwa matumizi ya Serikali, bado ni wa kiwango cha chini. Hali hii imesababisha kupungua kwa masoko ya bidhaa zinazozalishwa kwa kutumia malighafi za ndani, hivyo kuathiri uchumi wa taifa.

**Lengo**
Kuongeza ununuzi wa bidhaa na huduma zinazozalishwa kutokana na malighafi za hapa nchini.

**Tamko**
Serikali itachukua hatua za kukuza ununuzi wa bidhaa na huduma zinazozalishwa kwa kutumia malighafi za hapa nchini ili kukuza uchumi wa nchi.

### 3.1.6 Suala: Maendeleo ya Kada ya Ununuzi na Ugavi Serikalini

**Maelezo**
Maendeleo ya kada ya ununuzi na ugavi serikalini ni muhimu katika utekelezaji wa shughuli za ununuzi wenye tija. Kwa kuzingatia ukweli kwamba sehemu kubwa ya matumizi ya bajeti ya Serikali hufanyika kupitia ununuzi, suala la weledi, likijumuishwa na uwepo wa mazingira wezeshi ya utendaji kazi, ni muhimu katika kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa kwa ufanisi. Kama ilivyo kwa kada zingine, kukosekana kwa kada imara ya ununuzi na ugavi, ni jambo lenye madhara makubwa katika utekelezaji na pia kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa.

**Lengo**
Kuendeleza kada ya ununuzi na ugavi nchini

**Tamko**
Serikali itahakikisha kuwa inaimarisha uratibu wa maendeleo ya kada ya ununuzi na ugavi ili kuleta tija katika ununuzi wa umma.

### 3.1.7 Suala: Utawala bora

**Maelezo**
Utawala bora ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa. Utekelezaji wa utawala bora huhusisha masuala mbalimbali kama: uwajibikaji; uwazi na usawa; ufanisi na tija; uzingatiwaji wa Sheria; n.k ili kujenga ustawi wa jamii iliyo sawa. Katika ununuzi wa umma, utawala bora ni moja kati ya misingi muhimu inayosisitizwa katika utekelezaji wa majukumu ya ununuzi serikalini ili kupata thamani halisi ya fedha zilizotumika. Hata hivyo, utekelezaji wa utawala bora katika ununuzi si wa kuridhisha. Hii inatokana na ukiukwaji wa mara kwa mara wa misingi ya utawala bora kama ambavyo imekuwa ikibainishwa na taarifa mbalimbali za ukaguzi wa ununuzi nchini.

**Lengo**
Kuwa na mfumo wa ununuzi wa umma unaozingatia misingi ya utawala bora.

**Tamko la sera**
Serikali itahakikisha inasimamia misingi ya utawala bora katika utekelezaji wa ununuzi wa umma ili kuleta ufanisi katika ununuzi wa umma.

## 3.2 MASUALA MTAMBUKA

### 3.2.1 Suala: Uhifadhi wa Mazingira

**Maelezo**
Katika kipindi cha miaka ya 1990, zilifanyika jitihada za kuanzisha sera mbalimbali zenye kuzingatia uhifadhi wa mazingira. Sera hizo zilileta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo endelevu ulimwenguni. Hapa nchini, sheria na taasisi zilizo na wajibu wa kusimamia uhifadhi wa mazingira endelevu hazikutoa uzito wa athari za shughuli za ununuzi wa umma katika uhifadhi wa mazingira.

**Lengo**
Kuwa na mfumo wa ununuzi utakaozingatia uhifadhi wa mazingira.

**Tamko la sera**
Serikali itaweka mfumo wa ununuzi utakaosaidia kuepusha athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira.

### 3.2.2 Suala: Ushirikishwaji wa Makundi Maalum ya Jamii

**Maelezo**
Kumekuwa na ushiriki mdogo wa makundi maalum ya kijamii katika ununuzi wa umma. Makundi hayo ni kama; vijana, wazee, wanawake, wajasiriamali wadogo na watu wenye mahitaji maalum. Ushirikishwaji wa makundi haya katika ununuzi wa umma ni muhimu katika kuchangia ustawi wa makundi hayo ili kuleta usawa wa kijamii na kiuchumi kwa maendeleo ya Taifa.

**Lengo**
Kutoa fursa kwa makundi maalum ya jamii kushiriki kikamilifu katika zabuni za umma.

**Tamko la sera**
Serikali itahakikisha kunakuwepo na utaratibu wa ushirikishwaji wa makundi maalum ya kijamii katika zabuni za umma ili kuchangia ustawi wa makundi hayo.

# SURA YA NNE

## 4.0 MUUNDO WA KISHERIA

Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma ni matokeo ya mabadiliko ya kisekta yanayoendelea nchini. Lengo la mabadiliko hayo ni kujenga mfumo wa ununuzi wenye ufanisi na wa uwazi unaoendana na matakwa muhimu na ya msingi ya utawala bora. Moja ya vitu vilivyotoa msukumo katika hatua hii ni mahitaji ya haraka ya kuondoa upungufu wa mfumo wa ununuzi uliotawaliwa na sheria zisizotoshelevu. Hivyo, ni wazi kuwa zipo baadhi ya sheria ambazo zitahitaji kufanyiwa marekebisho ili kuendana na mahitaji halisi ya sasa.

Kwa sasa, muundo wa kisheria wa ununuzi wa umma unasimamiwa na sera pamoja na sheria mbalimbali zinazoendana na shughuli za ununuzi ikiwa ni pamoja na Sera ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi, Sera ya Taifa ya Nishati, Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi, Sheria ya Fedha za Umma, Sheria ya Bajeti, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sheria ya Uwekezaji, Sheria ya Serikali za Mitaa, Sheria ya Mikataba, Sheria ya Ushindani wa Haki, n.k.

**Muundo wa Udhibiti**

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma unamaanisha uchambuzi, uoanishaji na utungaji wa sheria zinazohusiana na ununuzi wa umma na udhibiti. Uzingatiaji wa sheria na kanuni za ununuzi wa umma ni jambo la msingi katika kuyafikia malengo ya ununuzi. Taarifa zote za ukaguzi wa ununuzi zinaonesha ukiukwaji wa sheria na kanuni kwa baadhi ya taasisi nunuzi.

Taarifa hizo zinaonesha kiwango kidogo cha uzingatiaji wa sheria ya ununuzi. Hivyo, Serikali inao wajibu wa kuhakikisha kiwango cha uzingatiaji wa sheria ya ununuzi kinaongezeka.

## SURA YA TANO

# 5.0 MUUNDO WA KITAASISI

## 5.1 Muundo wa Kiutekelezaji

Ununuzi wa umma ni suala mtambuka linalogusa wadau wa sekta zote, kwa msingi huo utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma utahusisha wadau mbalimbali. Wadau hawa ni pamoja na ; Wizara yenye dhamana ya usimamizi wa ununuzi wa umma, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma, Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Umma Serikalini, Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi, Taasisi Nunuzi, Sekta Binafsi na Taasisi za Mafunzo.

i) **Wizara yenye dhamana ya usimamizi wa ununuzi,** Itahusika kuratibu masuala yote yanayohusu kuandaa; Sera, Sheria, Taratibu, Kanuni, na Miongozo ya ununuzi wa umma pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sera. Wadau watakaoshiriki katika utekelezaji ni:-

ii) **Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA)**
Masuala yahusuyo uzingatiwaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya ununuzi wa umma yatafanywa na Mamlaka hii.

iii) **Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma (PPAA)**
Masuala yanayohusu malalamiko katika ushiriki wa zabuni za umma yatashughulikiwa na Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma.

iv) **Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA)**
Taasisi hii itatekeleza Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma kupitia ununuzi wa pamoja wa bidhaa na huduma mtambuka unaofanyika kwa mikataba maalum pamoja na huduma za ugomboaji wa mizigo.

v) **Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB)**
Bodi hii itatekeleza Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma kwa kuzingatia masuala ya maendeleo ya kitaaluma ya ununuzi na ugavi.

vi) **Taasisi Nunuzi (PE)**
Taasisi hizi zitawajibika kuitekeleza Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma kwa kufanya ununuzi utakaozingatia sheria, kanuni na miongozo ya ununuzi wa umma.

vii) **Sekta Binafsi**

Sekta binafsi itatekeleza Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma kwa kushiriki katika zabuni za umma, kutoa ushauri, kushiriki katika kujenga uwezo, kutoa mikopo, uzalishaji wa bidhaa, n.k.

viii) **Taasisi za Mafunzo**

Taasisi za mafunzo zitatekeleza sera hii kwa kuandaa mitaala mahsusi ya mafunzo ya ununuzi na ugavi nchini ili kukuza kiwango cha weledi na taaluma.

## 5.2 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na tathmini ni nyenzo muhimu katika kuweka utaratibu au mfumo wa kujenga msingi wa kutambua ufanisi katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ununuzi wa U mma. Vilevile unalenga kupata taarifa za utendaji na ufanisi ambazo zitatumika kufanya maamuzi muhimu ya kuboresha miongozo mbalimbali inayozielekeza taasisi nunuzi katika masuala yote yanayohusu ununuzi wa umma.

### 5.2.1 Lengo Kuu la Ufuatiliaji na Tathmini

Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ni muhimu kwasababu unalenga kutoa mwongozo wa utekelezaji wa sera hatua kwa hatua kwa ufanisi.

### 5.2.2 Ufuatiliaji

Ili kuhakikisha kuwa Sera ya Taifa ya ununuzi inatekelezwa kwa ufanisi, mfumo wa ufuatiliaji utekelezaji wa sera utaandaliwa na kutaratibiwa utekelezwaji wake na Wizara yenye dhamana ya usimamizi wa ununuzi wa umma. Inategemewa kuwa ufuatiliaji shirikishi utawezesha ufikiwaji wa utekelezwaji wa malengo ya jumla ya sera kwa jitihada za pamoja za wadau wote chini ya usimamizi wa wizara yenye dhamana ya usimamizi wa ununuzi nchini.

### 5.2.3 Tathmini

Tathmini itafanyika kila baada ya miaka mitano kwa lengo la kufahamu mwenendo wa utekelezaji wa sera ili kubaini upungufu uliopo pamoja na changamoto mpya zilizojitokeza wakati wa utekelezaji. Taarifa ya tathmini itatumika katika maandalizi ya mipango ya maendeleo ya sekta ya ununuzi wa umma. Hivyo, wizara yenye dhamana ya usimamizi wa ununuzi wa umma itaandaa utaratibu wa kutathmini ufanisi wa mfumo wa ununuzi nchini huku na kuendelea kurekebisha maeneo yote yatakayobainika kuhitaji maboresho.

## 5.3 Hitimisho

Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma itatoa muongozo utakaowezesha Taifa kunufaika kwa mchango utakaotokana na sekta ya ununuzi. Sera hii inaweka misingi endelelevu yenye kulinda maslahi ya Taifa. Hivyo, imezingatia kuwepo kwa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II), Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2016/17 - 2020/21 na Sera na Mtambuka.